



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA  
HABARI



## TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

TAARIFA YA UMMA: MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI  
TANZANIA

### Maelekezo kwa Makampuni na Mashirika Yote Yanayofanya Kazi Tanzania

Kutokana na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya 2022, Tume inyakumbusha makampuni, taasisi na mashirika yote kwamba hatua zozote zinazohusiana na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi zinapaswa kufanywa kwa kuzingatia umakini na kufuata sheria husika na mipango ya Tume. Ili kuhakikisha jukumu la kulinda taarifa binafsi linafanyika kwa usahihi, ni muhimu kwa taasisi zote kufuata mwongozo kutoka Tume (PDPC).

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ndiyo yenye jukumu la kuratibu na kusimamia masuala ya ulinzi wa taarifa binafsi nchini na hutoa miongozo kwa taasisi zote kutimiza majukumu yao ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa ufanisi. Aidha, Tume inaelekeza makampuni na mashirika kushirikiana na makampuni na watu binafsi waliothibitishwa na wanaojulikana na Tume kwa huduma zozote zinazohusiana na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Kwa kufanya kazi na wataalamu waliothibitishwa na Tume, tunahakikisha hatua za ulinzi wa taarifa binafsi ziko katika mkondo wa mahitaji ya kisheria na malengo ya Tume kwa mujibu wa Sheria na mpango wa usimamizi ulivyopangwa.

Kwa maelezo zaidi na mwongozo kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, wasiliana na Tume kwa anwani iliyo chini.

**"FARAGHA YAKO NI WAJIBU WETU"**

Mkurugenzi Mkuu,  
Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi,  
S. L. P. 1105,  
Jengo la UCSAF,  
Barabara ya 10,  
41107 Dodoma.  
Barua-pepe: dg@pdpc.go.tz